

# **MTIHANI WA MWIGO WA PTE 2019**

## **KISWAHILI 1013/1**

### **MUDA: SAA 2**

#### **MAAGIZO**

- a) Mtihani huu una sehemu **NNE** muhimu: Insha, Ufahamu, Matumizi ya Lugha na Sajili ya Lugha.
- b) Ni muhimu sana ufuate maagizo uliyopewa mwanzoni mwa kila sehemu.
- c) Andika majibu yako kwa Kiswahili sanifu.

#### **KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

<b>SEHEMU</b>	<b>SWALI</b>	<b>UPEO</b>	<b>ALAMA</b>
<b>A – LUGHA</b>			
Insha	01	20	
Ufahamu	02	20	
Sarufi	03	30	
Msamiati	04	20	
Sajili ya Lugha	05	10	
<b>JUMLA</b>		<b>100</b>	

#### **SEHEMU YA KWANZA**

##### **INSHA**

**(alama 20)**

1. Andika insha isiyopungua maneno 350 kuhusu mojawapo ya mada zifuatazo.

- a) Andika maagizo kwa wanafunzi kuhusu udurusi au jinsi ya kujiandaa kwa ajili ya mtihani wa darasa la nane.
- b) Ukosefu wa usalama ni tatizo sugu katika nchi yetu. Jadili.
- c) Mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu. Thibitisha ukweli wa methali hii.
- d) Malizia kwa ..... Lo! Mungu ni mkubwa.

#### **UFAHAMU**

Kushamiri kwa wimbi la uonyeshaji ponografia kuna athari kubwa kwa jamii hususan kwa vijana. Ingawa watu wengine hudai picha hizi haziwaathiri upo ushaidi tumbi nzima unaoonyesha kuwa wanaotazama pich za ngono hupata matatizo. Lazima ielewke kuwa kinachoonekana na jicho au kusikika kwa sikio huathiri fikira au hisia. Picha za matusi

zinachangia kwa kiasi kikubwa kuharibu akili. Badala ya kuzingatia mambo muhimu kama masomo, watu huanza kutafakari mambo machafu.

Vijana wengi ni kama bendera. Hivyo basi wao huanza kuiga wanayoyaona na kusikia. Hili ni tatizo linalowafanya kuacha mkondo wa maadili. Kutokana na uchafu huu, wengi wao hushawishiwa kuingilia shughuli za ngono mapema kabla hawajakomaa kimwili, kiakili na kihisia. Bidhaa yake ni pamoja na ukahaba, utendaji mbaya sheleni, mahudhurio mabaya darasani na mimba zisizotarajiwa. Vijana wengi huacha shule kabisa. Wengine nao huambukizwa magonjwa ya zinaa ambayo huwaletea mauti.

Inasemekana kuwa akili za binaadamu hunasa zaidi mambo yanayowasilishwa kwa picha. Si ajabu, vijana huyadumisha matusi haya katika kumbukumbu zao na kuyafanya sehemu ya maisha yao. Wengi wao huanza kuandama tabia mbovu kama ushoga, ubasha na usagali. Aidha, vijana kwani wanaiga mitindo mibaya ya mavazi yanayoanika uchi wao. Hali kadhalika huiga lugha, ishara na miondoko inayohusiana na ngono. Yote haya yanapingana na desturi za mwaafrika. Si ajabu visa vya ubakaji vinaongezeka kila leo. Utazamaji wa picha chafu aghalabu huandamana na maovu mengine kama unywaji wa pombe, matumizi ya dawa za kulevyo, uvutaji sigara na utumiaji wa dawa za kuchochaea uchu wa ngono. Mambo haya huwapa vijana tabia za uhayawani. Jambo hatari ni kuwa kuendelea kutazama picha hizi huzifanya nishai na hisia za watu kuwa butu, yaani kuondoa makali. Hata katika utu nzima, mtu atapoteza mhemko wa kawaida na kugeuzwa kuwa mtegemezi wa ponografia. Tatizo hili linaenea kwa vishindo mijini and vijijini. Aihasili ponografia imechangia pakubwa kuenea kwa haya.

Ipo haja ya dharura kukinga jamii kutokana na maenezi haya yasiyo na kuzuizi. Jambo la kwanza ni kuongeza ufahamu wa umma wote kuhusu uovu wa picha hizi. Ufahamu huu utaweza kupunguza mahitaji na uuzaji wa ponografia. Aidha ni vizuri watu wazima wawajibike ili wawalind vijana kutokana na athari hizi. Inapasa wenye midahlishi, tovuti, video na cinema kuwazuia vijana kutazama uchafu huu. Kwa kuwa tatizo la kuenea kwa ponografia limeendelea kuwepo kwa sababu ya udhaifu wa sharia, pana dharura ya kuweka sharia za kuzuia utennezaji wa upungufu huu. Kuambatana na haya, hatua kali zichukuliwe kwa wanovunja sharia hizi. Hali kadhalika, ushirikiano wa karibu baina ya wadau uimarishwe katika ulimwengu mniza. Serikali na mashirika ya midahilishi yajuike kutambua chanzo cha taka hizi kisha wanaohusika wakabiliwe ipasvyo. Jamii ingependwa kuona michakato ya kuharamisha usambazaji na utangazaji wa ponografia ikiwekwa.

Wazazi nao wasijipweteke tu bali nao wawajibike. Ni muhimu washikilie kwa dhati juhudhi zao za kuwaelekeza na kuwashauri watoto kuzingatia oungofu wa kukwepa picha hizi najisi. Watoto lazima waeleweshwe kuwa haifai kutazama picha au michoro michafu. Itikadi na imani za kidini na utamaduni wa kiafrika zinakataza vikali mtu kuona

uchi wa mtu mwingine. Matokeo ya kuasi makatazo haya yana madhara makubwa kwa watu wa jamii.

- (a) Kipewe kifungu hiki anwani mwafaka. (alama 1)
- (b) Kulingana na kufungu hiki, nini ponografia? (alama 1)
- (c) “Vijana wengi ni kama bendera”. Fafanua huku ukitoa mifano kutoka kwenye taarifa uliyosoma. (alama 5)
- (d) Ni zippi athari za kudumu zinazosababishwa na utazamaji wa ponografia? (alama 4)
- (e) Kutokana na taarifa, jamii inaweza vipi kujikinga na mabaya ya ponografia? (alama 3)
- (f) Eleza mchango wa serikali katika kupiga vita ponografia katika jamii. (alama 2)
- (g) Eleza maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa.  
(alama 3)
- i) Bidhaa \_\_\_\_\_
- ii) Najisi \_\_\_\_\_
- iii) Shamiri \_\_\_\_\_

### **3. MATUMIZI YA LUGHA (alama 50)**

- (a) Taja sifa bainifu za sauti hizi /th/ /na/ /dh/ (alama 2)
- (b) Maneno haya hupatikana katika ngeli gani. (alama 2)
- i) Waraka \_\_\_\_\_
- ii) Kofi \_\_\_\_\_
- (c) Ainisha kitenzi kilichopigwa mstari katika sentensi zifuatazo. (alama 2)
- i) Osiepa alikuwa mchangamfu
- ii) Osiepa alikuwa akishiriki
- (d) Andika kwa udogo ukitumia “O” rejeshi.  
(alama 2)

Runinga ambayo ilinunuliwa imeangukiwa na mti wetu.

- (e) Bainisha aina ya shamirisho katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Kidani anampikia Amina chakula kwa birika.

- (f) Onyesha matumizi ya kwa katika sentensi hii. (alama 3)

Licha ya kusafiri kwa ndege, alituhumiwa kwa kusahau cheti chake.

- (g) Afikisha sentensi ifuatayo ili itoe maana tofauti. (alama 2)

Mkulima hajavuna chochote.

- (h) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (alama 2)

W+T+N+E

- (i) Tunga sentensi ukitumia parandesi. (alama 2)

- (j) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi. (alama 3)

Mtoto mwerevu alipata zawadi nono

- (k) Unda nomino moja moja kutokana na vitenzi. (alama 4)

i) Hesabu \_\_\_\_\_

ii) Poromoka\_\_\_\_\_

iii) – la \_\_\_\_\_

iv) – fa \_\_\_\_\_

(l) Tumia – zuri kama kiwakilishi, kielezi na kivumishi katika sentensi moja. (alama 3)

4. (a) Hamisi ni mmewe Kudra. Waadi ni mkewe Lindo. Kudra na Lindo ni ndugu wana watoto. (alama 5)

i) Nani mwanyumba \_\_\_\_\_

ii) Nani shangazi \_\_\_\_\_

iii) Watoto wa Kudra na Waadi wataitanaje? \_\_\_\_\_

iv) Waadi na dadake Lindo wataitanaje? \_\_\_\_\_

(b) Kamilisha methali. (alama 2)

i) \_\_\_\_\_ ni uongo wa mpita njia.

ii) Kipendacho moyo \_\_\_\_\_

- (c)i) Malipo anayopewa mtu ili kumkuliza hasira \_\_\_\_\_ (alama 2)
- ii) Malipo anayopewa mtu kwa kuokota kitu \_\_\_\_\_ (alama 2)
- (d)i) Msimamizi mkuu wa shamba huitwa \_\_\_\_\_ (alama 1)
- ii) Msimamizi mdogo wa shambani huitwa \_\_\_\_\_ (alama 1)
- (e) Chora maumbo haya. \_\_\_\_\_ (alama 3)
- i) Mche duara
- ii) Mstatili
- iii) Duara Dufu
- (f) Eleza maana ya nahau zifuatazo. \_\_\_\_\_ (alama 4)
- i) Kuvulia mtu miwani
- ii) Kutia chumvi

#### **4. SAJILI YA LUGHA** \_\_\_\_\_ (alama 10)

Benki yenewe haina kitu ..... CD4 count yake iko chini ..... Ni  
emergency ..... Tutampoteza ikikosekana.

- i) Hii ni sajili ya aina gani? \_\_\_\_\_ (alama 2)
- ii) Fafanua sifa **nne** zinazohusishwa na sajili hiyo. \_\_\_\_\_ (alama 8)